**TAARIFA YA MANUNUZI ROBO YA PILI (OKTOBA – DISEMBA) 2016/2017**
Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa ya Manunuzi robo ya pili (Oktoba – Disemba).Taarifa iliainisha Manunuzi mbalimbali yaliyofanyika katika kipindi husika ikiwa ni pamoja na kuonyesha utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa kupitia vikao mbalimbali vya Bodi ya Zabuni ya Halmashauri.

**A: TAARIFA ZA MANUNUZI YALIYOFANYIKA KUPITIA VIKAO VYA BODI YA ZABUNI YA HALMASHAURI:**
Taarifa ilieleza kuwa katika kipindi cha robo ya pili Bodi ya Zabuni ya Halmashauri imeutana mara tatu na kufanya/kupitisha kazi zifuatazo;

**KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 15.10.2016**

**(i) KUPITIA NA KUIDHINISHA NYARAKA ZA KUTANGAZA KAZI ZA BARABARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA KUIDHINISHA NJIA YA MANUNUZI ITAKAYOTUMIKA**

Taarifa ilieleza kuwa Bodi ya Zabuni ilipokea nyaraka za kutangaza kazi za barabara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kuzipitia kwa umakini. Wajumbe wa bodi walitaka kujua bajeti ya kila barabara kama ilivyo kwenye mpango wa manunuzi hivyo na hivyo katibu aliwasilisha bajeti hiyo.
Baada ya maajadiliano ya kina pamoja na marekebisho madogo yaliyofanyika wajumbe wa Bodi waliidhinisha nyaraka hizo kwa ajili ya kutangaza kazi tajwa hapo juu kwa kutumia njia ya Zabuni Kitaifa.

Pia wajumbe wa bodi walitoa maoni ya jumla kwa ajili ya kuboresha taarifa kwa kazi za matengenezo ya barabara kwa kipindi hiki na kwa kipindi kijacho kama ifuatavyo;-

- Kuwe na taarifa inayoonyesha maeneo yatakayofanyiwa kazi za matengenezo ya barabara sababu jina la mradi huwa linataja barabara nzima bila kuonyesha eneo litakalotengenezwa ili wajumbe wapate kujua pia kuepuka kurudiwa kutengenezwa sehemu moja.
- Wajumbe walishauri kuwa mhandisi aweke muda wa kazi zinazotangazwa ili utumike kuwapima wazabuni watakaomba kazi.
- Pia wajumbe walisema kama kunauwezekano wakuiombea barabara ya Kiangara/Kitogoro/Mtawatawa ibadilishwe jina ibakie Kiangara/Kitogoro sababu mtawatawa inaanzia kwenye daraja katika barabara ya Tanroad.

**Utekelezaji:**
Zabuni za barabara 2016/2017 zilikwisha tangazwa katika gazeti la habari leo la tarehe 27.10.2016

**(ii) KUPOKEA TAARIFA YA UCHAMBUZI NA KUPITISHA MKANDARASI WA KAZI YA KUENDELEZA MRADI WA UMWAGILIAJI KATIKA KIJIJI CHA MTAWANGO, KATA YA MBAYA**

Taarifa ilieleza kuwa Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia. Baada ya majadiliano ya wajumbe walimpitisha mkandarasi Almas General Supplies, S.L.P 131, SONGEA kwa gharama ya Tshs 326,213,921.94 kwa muda wa miezi sita. Pia wajumbe waliagiza wakati wa utekelezaji wa mradi huo mkandarasi alete taarifa za mtaalamu atakayekuwa anasimamia Mradi huo kwa jina.

**Utekelezaji:**
Halmashauri inasubiri maamuzi kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ili kuendelea na hatua zinazofuata.

**(iii) MAOMBI YA KUTENGENEZA BARABARA YA LIPALA - NYERA KATIKA KATA YA KICHONDA**

Afisa mipango aliwasilisha maombi ya matengenezo ya barabara ya Lipala - Nyera katika kata ya Kichonda baada ya kuwasilisha wajumbe wa bodi walishauri kuwa Mhandisi wa ujenzi aandae makisio ya barabara hiyo ili yaweze kuwasilishwa katika kikao kijacho cha menejimenti kwa ajili ya majadiliano.

**Utekelezaji:** Makisio yalikwisha andaliwa na kuwasilishwa kwenye kikao cha Menejimenti.

**<u>KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 21.10.2016</u>**

**(i) KUPITIA NA KUJADILI USHAURI WA AFISA MASUULI KUHUSIANA NA MAAMUZI YA KIKAO CHA BODI CHA TAREHE 15.10.2016**

Taarifa ilieleza kuwa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ilikutana katika kikao maalumu ili kuanzisha majadiliano ya upunguzaji gharama za mradi kwa mkandarasi aliyepitishwa na Bodi ya Zabuni ya Halmashauri kwa kuzingatia taarifa ya uchambuzi wa kazi husika kufuatia maagizo ya Afisa Masuuli aliyoyatoa kwa mujibu wa Kanuni ya 51(a) ya sheria za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.
Baada ya wajumbe kupitia hoja zilizowasilishwa na Katibu wa Bodi, Bodi ilimshauri Afisa Masuuli kutumia Kanuni ya 51(b) ya sheria za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 inayosema " iwapo Afisa Masuuli ana mashaka juu mapitio ya Bodi ya Zabuni anaweza kuomba mapitio huru kutoka Mamlaka ya udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA).
**Utekelezaji:**
Barua ya kuwasiliana na PPRA ilikwisha andikwa tarehe 27.10.2016 na nyaraka husika zilipelekwa tarehe 28.11.2016.

**<u>KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 14.12.2016</u>**

(i)Bodi ya Zabuni ilipokea taarifa ya uchambuzi wa kazi za matengenezo ya barabara 2016/2017 na kufanya maamuzi yafuatayo;

**a) MATENGENEZO YA MUDA MAALUM,SEHEMU KOROFI NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA LIWALE/KIKULYUNGU, NA MATENGENEZO YA KAWAIDABARABARA YAMBAYA/KICHONDAMBAYA/NAMIHU/MAKATA**

**YAMBAYA/KICHONDAMBAYA/NAMIHU/MAKATA.ZABUNI NA:LGA/054/2016/2017/W/65**

Bodi ya Zabuni ilipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia. Baada ya majadiliano ya muda wajumbe walimpitisha mkandarasi Mahabu Company Ltd, S.L.P 7777,Mwanza kwa gharama ya Tshs 81,449,500/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 90.

b) **MATENGENEZO YA MUDA MAALUM,SEHEMU KOROFI NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA LIWALE/LILOMBE/MBWEMKURU NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA NGUNJA/NAHORO NA KIPULE/MANGIRIKITI ZABUNI NA: LGA/054/2016/2017/W/66**

Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia. Baada ya majadiliano wajumbe walimpitisha mkandarasi Norcom (T) Ltd, S.L.P 621, Lindi kwa gharama ya Tshs 123,158,960/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 90.

c) **MATENGENEZO YA MUDA MAALUM,SEHEMU KOROFI NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA KIANGARA/MIRUI NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA MIRUI/MBWEMKURU NA KIANGARA/KITOGORO/MTAWATAWA ZABUNI NA: LGA/054/2016/2017/W/67**

Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia . Baada ya majadiliano ya muda wajumbe walimpitisha mkandarasi Litopite Construction Company, S.L.P 92, Liwale kwa gharama ya Tshs 77,533,080/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 90.

d) **UKARABATI WA DARAJA LA NAMBINDA KATIKA BARABARA YA MAKATA/NDAPATA ZABUNI NA: LGA/054/2016/2017/W/68**

Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia . Baada ya majadiliano ya muda wajumbe walimpitisha mkandarasi Likecha Construction Company Ltd, S.L.P 29, Liwale kwa gharama ya Tshs 131,337,256.80/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 135.

e) **MATENGENEZO YA MUDA MAALUM NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA LIWALE MJINI NA MATENGENEZO YA MUDA MAALUM BARABARA YA UKANDA WA UWANJA WA NDEGE ZABUNI NA: LGA/054/2016/2017/W/69**

Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia. Baada ya majadiliano ya muda wajumbe walimpitisha mkandarasi Samoma Investment Co.Ltd, S.L.P 144, Liwale kwa gharama ya Tshs 90,195,660/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 90.

f) **MATENGENEZO YA MUDA MAALUM, SEHEMU KOROFI NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA NANGANO/NAHORO, MATENGENEZO YA MUDA MAALUM NA**

**MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA KIBUTUKA/NGUMBA ZABUNI NA: LGA/054/2016/2017/W/70**

Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia. Baada ya majadiliano ya muda wajumbe walimpitisha mkandarasi Saljos Contractors Ltd, S.L.P 71921, Dar es salaam kwa gharama ya Tshs 78,570,890/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 90.

g) **MATENGENEZO YA MUDA MAALUM, SEHEMU KOROFI NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA LIWALE/MPIGAMITI ZABUNI NA: LGA/054/2016/2017/W/71**

Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia. Baada ya majadiliano ya muda wajumbe walimpitisha mkandarasi Namacoy Construction Co. Ltd, S.L.P 50, Newala kwa gharama ya Tshs 64,050,000/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 90.

h) **MATENGENEZO YA MUDA MAALUM, SEHEMU KOROFI NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA MAKATA/NDAPATA ZABUNI NA: LGA/054/2016/2017/W/72**

Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia. Baada ya majadiliano ya muda wajumbe walimpitisha mkandarasi Liwale Investment Co. Ltd, S.L.P 46, Liwale kwa gharama ya Tshs 77,671,140/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 90.

i) **MATENGENEZO YA MUDA MAALUM, NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA LIWALE/BARIKIWA, MATENGENEZO YA MUDA MAALUM NA MATENGENEZO YA KAWAIDA BARABARA YA MAKATA/MKUNDI/KIGWEMA ZABUNI NA: LGA/054/2016/2017/W/73**

Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia kwa umakini na baada ya majadiliano ya muda wajumbe walimpitisha mkandarasi Africa Oner Co. Ltd, S.L.P 35591,Dar es salaam kwa gharama ya Tshs 67,727,275/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 90.

j) **MATENGENEZO YA MUDA MAALUM BARABARA ZA LIWALE MJINI (KATA YA NANGANDO 4KM, KATA YA LIKONGOWELE 4KM NA LIWALE MJINI 2KM) ZABUNI NA: LGA/054/2016/2017/W/74**

Wajumbe wa bodi walipokea taarifa ya uchambuzi na kuipitia. Baada ya majadiliano ya muda wajumbe walimpitisha mkandarasi J.P Traders Ltd S.L.P 76007,Dar es salaam kwa gharama ya Tshs 286,774,928/= pamoja na VAT kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 120.

**Utekelezaji:**

Barua za kuwataarifu waliokosa kazi na sababu zilizopelekea zilikwisha andikwa tarehe 19/12/2016. Aidha barua za kuwataarifu wale wote waliopata kazi zilitolewa

tarehe 30.12.2016 na kwa sasa wanashughulikia suala la bima ndipo mikataba isainiwe.